# GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**14 AGOSTI 2026**

*Hupigwa Chapa kwa Idhini ya Serikali na Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti* — *Hutolewa kila Ijumaa*

*Bei Tshs .3000/=* — **CXXXV Nam. 7517**


**YALIYOMO** *Ukurasa*


Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar, Nam.7 ya 1997.
Kanuni za Tume ya Utangazaji Zanzibar (Maudhui ya Utangazaji), 2026.


**SEHEMU YA SHERIA**

Sheria zilizotajwa hapo chini zimetangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

**Tangazo la Sheria**

Nam.73:-Kanuni za Tume ya Utangazaji Zanzibar (Maudhui ya Utangazaji), 2026.

---

**TANGAZO NAM. 73**

## SHERIA YA TUME YA UTANGAZAJI ZANZIBAR, NAM. 7 YA 1997

## KANUNI ZA TUME YA UTANGAZAJI ZANZIBAR (MAUDHUI YA UTANGAZAJI), 2026

### MPANGILIO WA KANUNI

**KANUNI** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**UTANGULIZI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**WAJIBU WA MTOA HUDUMA ZA UTANGAZAJI**

3. Wajibu wa mtoa huduma za utangazaji wa umma.
4. Wajibu wa mtoa huduma za utangazaji wa biashara.
5. Wajibu wa mtoa huduma za utangazaji zisizo za biashara.
6. Wajibu wa mtoa huduma za utangazaji wa jamii.

**Matangazo yaliyohusu Waliofariki na Mali wa Watu waliofariki, kuvunja Mikataba ya ushirikiano, taarifa za Makampuni, Upotevu na marekebisho ya Nyaraka za Serikali na mengineyo ambayo ni muhimu kwa Umma lazima kuchapishwa katika Gazeti Rasmi. Nakala za Matangazo hayo zipelekwe kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania SLP 261 Maruhubi, Zanzibar. Nakala ziwasilishwe kabla ya Siku ya Alhanisi ya kila Wiki**

7. Wajibu wa mtoa huduma za Utangazaji wa kulipia.
8. Wajibu wa mtoa huduma za maudhui ya mtandaoni.

**SEHEMU YA TATU**
**MASHARTI YA UTOAJI NA UTENGENEZAJI WA MAUDHUI**

9. Msambazaji wa maudhui.
10. Masharti ya Jumla.
11. Wajibu wa mwenye leseni kulinda mtoto.
12. Maudhui ya watu wazima.
13. Uwasilishaji wa Habari.
14. Habari za papo kwa papo.
15. Matukio.
16. Utoaji wa maoni binafsi.
17. Mwenendo wa Baraza la Wawakilishi na Bunge.
18. Mwenendo wa Mahkama.
19. Matangazo ya biashara.
20. Habari za biashara.
21. Maudhui kwa ajili ya watu wenye ulemavu.
22. Maudhui ya elimu.
23. Kuripoti masuala yenye migogoro.
24. Mahojiano.
25. Katazo kwa mwenye leseni.
26. Maudhui ya ndani.
27. Wajibu wa Mtengenezaji wa maudhui.

**SEHEMU YA NNE**
**MAADILI YA VIPINDI**

28. Maadili ya vipindi.
29. Matukio yenye maslahi ya Taifa.
30. Kutaja jina la kituo na mtayarishaji wa kipindi.
31. Taarifa za uchunguzi.
32. Faragha.
33. Vipindi vinavyorushwa hewani moja kwa moja.
34. Matumizi ya akiliunde.
35. Utazamaji wa vipindi na familia.
36. Ratiba ya vipindi.
37. Ubaguzi.
38. Sera ya uhariri.

**SEHEMU YA TANO**
**MASHARTI YA JUMLA**

39. Dharura za umma.
40. Uvunjaji wa Kanuni.
41. Ubebaji wa huduma za utangazaji wa umma.
42. Uthibitisho wa haki.
43. Masharti kwa ajili ya haki za kipekee.
44. Malalamiko.
45. Makosa na adhabu.

46. Uwezo wa kumaliza.
47. Utaratibu wa kumaliza.
48. Rufaa.

**MAJADWELI**

**TANGAZO NAM. 73**

**SHERIA YA TUME YA UTANGAZAJI ZANZIBAR, NAM. 7 YA 1997**

---

**KANUNI ZA TUME YA UTANGAZAJI ZANZIBAR (MAUDHUI YA UTANGAZAJI), 2026**
**[Chini ya kifungu cha 29(1)]**

---

**KWA UWEZO** niliopewa chini ya kifungu cha 29 (1) cha Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar, Nam.7 ya 1997, Mimi, **DRT. RIZIKI PEMBE JUMA,** Waziri wa Habari, Sanaa Utamaduni na Michezo, natunga Kanuni zifuatazo:

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Tume ya Utangazaji Zanzibar (Maudhui ya Utangazaji), 2026 na zitaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Waziri na kutangazwa katika Gazeti Rasmi.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"akiliunde" maana yake nadharia ya uundaji wa mifumo ya kompyuta na teknolojia yenye uwezo wa kutekeleza kazi ambazo kwa kawaida zinahitaji akili ya binadamu kama kuona, kutambua sauti, kufanya maamuzi na kutafsiri lugha.

"habari biashara" maana yake ni utangazaji wa zaidi ya dakika moja unaloelezea kwa undani bidhaa au huduma ikijumuisha maonesho ya matumizi ya bidhaa na utoaji wa ofa unaomuwezesha mtangazaji kupata malipo ya fedha au ya aina nyengine;

"huduma za utangazaji" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika sheria;

"huduma za maudhui" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika sheria;

"huduma za maudhui ya biashara" maana yake ni huduma za maudhui zinazogharamiwa kwa ajili ya kupata faida;

"huduma za maudhui ya jamii" maana yake ni huduma za maudhui zinazotolewa katika jamii husika bila ya malipo;

"huduma za maudhui ya umma" maana yake ni aina ya huduma za utangazaji zinazotolewa kwa ajili ya umma, zinazofadhiliwa na umma na zisizo ingiza faida;

"huduma za utangazaji wa kulipia" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria;

"kipindi" maana yake ni maudhui ya matangazo ya moja kwa moja au yaliyorekodiwa yenye picha, sauti au vyote kwa pamoja yanayorushwa kwa madhumuni ya kutangazwa au kuoneshwa kwa umma;

"leseni" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria;

"matukio yenye maslahi kitaifa" maana yake matukio ya michezo, kisiasa serikali au mengineyo ambayo yana maslahi au umuhimu kwa jamii ya Zanzibar;

"matukio" maana yake ni matukio ya kihabari ambayo yanakwenda na wakati;

"maudhui ya kipindi" maana yake ni madhumuni ya kipindi kinachooneshwa au kutangazwa kwa jamii;

"muda wa faragha" maana yake ni muda wa utangazaji kuanzia saa sita usiku hadi saa kumi na moja alfajiri ambao Mwenye leseni atatangaza mambo yanayofaa kwa ajili ya watu wazima;

"msambazaji wa maudhui" maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria;

‘‘mtangazaji‘‘ maana yake kama ilivyotafsiriwa katika Sheria;

‘‘mtengenezaji maudhui‘‘ maana yake ni mtu anayebuni na kutengeneza maudhui kwa ajili ya matumizi ya kidijitali kwa lengo la kuelimisha, kuburudisha, kushawishi au kuuza bidhaa/huduma;

"mteja" maana yake ni mtu aliyeingia makubaliano na Mwenye leseni ya huduma za maudhui ya kulipia kwa ajili ya upatikanaji wa maudhui kwa kulipa ada;

"mtoto" maana yake ni mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na nane;

"mwenye leseni" maana yake ni mtu yeyote aliyepewa leseni na Tume kutoa huduma za maudhui;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar, Nam. 7 ya 1997;

"Sera ya uhariri" maana yake ni mfumo wa maudhui unaoelezea maoni, msimamo, nafasi ya kituo ikiwa ni pamoja na wahariri wake juu ya malengo, aina za maudhui, hadhira iliyokusudiwa, na masuala mengine yoyote;

"tangazo la biashara" maana yake ni utangazaji kwa malipo usiozidi dakika moja kwa madhumuni ya:

(a) kuuza bidhaa au huduma yoyote;
(b) kushawishi hadhira kuhusu imani au tukio; au
(c) kukuza bidhaa, huduma, mtu au shirika.

"taarifa" maana yake ni taarifa kwa umma juu ya kitu kilichotokea, kinachotokea au kitakachotokea;

"Tume" maana yake ni Tume ya Utangazaji Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 5 cha Sheria;

"ubebaji wa huduma za Utangazaji wa umma" " maana yake ni ulazima kwa msambazaji wa maudhui kubeba huduma ya utangazaji wa umma kumfikia mtumiaji bila ya kutoza gharama za urushaji kwa mtangazaji wa huduma za umma na ada kwa watumiaji;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na habari.

## SEHEMU YA PILI
## WAJIBU WA MTOA HUDUMA ZA UTANGAZAJI

Wajibu wa mtoa huduma za utangazaji wa umma.

**3.-**(1) Mtoa huduma za utangazaji wa umma atakuwa na wajibu wa:

(a) kutoa taarifa, elimu na burudani kwa umma kwa uhuru na bila ya upendeleo kwa kuzingatia mila silka na utamaduni wa Mzanzibari;
(b) kutoa huduma za matangazo kwa watu wote kwa kuzingatia maslahi na mustakabali kwa jamii yote ya Zanzibar;
(c) kupokea na kurusha hewani maudhui kutoka kwa watayarishaji wa kujitegemea na watu wengine kwa kuzingatia masharti ya chombo cha umma;
(d) kutoa vipindi vinavyokuza amani na utulivu, umoja wa kitaifa na ambavyo havihatarishi usalama wa Taifa;
(e) kutoa vipindi vinavyohamasisha kukuza na kulinda utamaduni, mila, silka na desturi za kizanzibari;
(f) kutangaza matokeo muhimu ya kitaifa na dharura za umma; na
(g) kufanya jambo lolote muhimu kwa maslahi ya Taifa kwa mujibu wa Sheria.

(2) Mtangazaji wa huduma za umma anayekusudia kutoa huduma utangazaji wa biashara:

(a) atakuwa na chaneli maalumu kwa ajili ya kutoa huduma za maudhui ya biashara;
(b) ataomba leseni ya huduma za utangazaji wa biashara kwa Tume kwa utaratibu ulioainishwa katika Sheria na Kanuni za Utoaji Leseni za Utangazaji;
(c) atatunza na kuweka hesabu tofauti kwa huduma zake za maudhui ya umma na biashara;
(d) atabainisha vipindi vilivyodhaminiwa na ambavyo havijadhaminiwa;

(e) atatoa vipindi vinavyokuza amani na utulivu, umoja wa kitaifa na ambavyo havihatarishi usalama wa Taifa;
(f) atatoa vipindi vinavyohamasisha kukuza na kulinda utamaduni, mila, silka na desturi za kizanzibari;
(g) ataepuka kutangaza masuala ya kashfa, ubaguzi na uchochezi;
(h) atalinda mtoto dhidi ya maudhui hatarishi ya vipindi yanayoweza kumuathiri au kumdhalilisha;
(i) ataepuka vipindi vinavyohusiana na uhamasishaji wa ngono, utupu, matusi, ulevi, kamari, vurugu, ushirikina na unajimu; na
(j) atafanya jambo lolote muhimu kwa maslahi ya Taifa kwa mujibu wa Sheria.

Wajibu wa mtoa huduma za utangazaji wa biashara.

**4.** Mtoa huduma za utangazaji wa biashara atakuwa na wajibu wa:

(a) kutangaza vipindi vinavyoakisi utamaduni, mahitaji na matarajio ya Zanzibar;
(b) kutoa huduma katika mawanda yaliyokubaliwa na Tume;
(c) kujumuisha vipindi ambavyo vitaakisi tunu na utambulisho wa utamaduni wa Mzanzibari;
(d) kukuza matumizi sanifu ya ugha za Kiswahili na Kiingereza;
(e) kutangaza vipindi vinavyokuza amani, utulivu na umoja wa kitaifa na ambavyo havihatarishi usalama wa Taifa; na
(f) kutoa huduma kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika leseni.

Wajibu wa mtoa huduma za utangazaji wa jamii.

**5.** Mtoa huduma za utangazaji zisizo za biashara atakuwa na wajibu wa:

(a) kutoa vipindi vinavyoendana na malengo mahsusi ya kuanzishwa kwa kituo chake;
(b) kuzingatia kikamilifu vigezo vya kitaaluma na maadili ya waandishi wa habari vinavyohitajika katika uwasilishaji wa habari;
(c) kukuza matumizi sanifu ya lugha za Kiswahili na Kiingereza; na
(d) kutoa huduma kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika leseni.

Wajibu wa mtoa huduma za utangazaji zisizo za biashara.

**6.** Mtoa huduma za utangazaji wa jamii atakuwa na wajibu wa:

(a) kutoa huduma za utangazaji zinazoakisi mahitaji ya watu kwa jamii husika, ikijumuisha mahitaji ya kitamaduni, kidini, kisiasa, na kiuchumi;
(b) kutangaza vipindi vinavyohusisha jamii husika ambavyo kwa kawaida havitolewi na watoa huduma wengine;
(c) kutoa huduma za utangazaji ndani ya eneo lililoidhinishwa na Tume;
(d) kutangaza vipindi vinavyotoa habari, elimu na burudani kwa jamii iliyokusudiwa;
(e) kutokujihusisha na uhusiano wa kisiasa na kidini utakaoathiri malengo ya leseni yake;

(f) kujikubalisha kukuza amani, utulivu, umoja wa kitaifa na utambulisho wa utamaduni wa jamii husika;
(g) kuhakikisha kwamba maudhui yaliyotolewa yanakidhi maslahi ya umma, tunu za kitaifa, usalama wa Taifa na umoja wa kitaifa; na
(h) kufuata kanuni za maadili ya uendeshaji wa huduma za utangazaji kwa jamii kama zitakavyotolewa na Tume.

Wajibu wa mtoa huduma za utangazaji wa kulipia.

**7.-**(1) Mtoa huduma za utangazaji wa kulipia atakuwa na wajibu wa:

(a) kurusha hewani angalau asilimia thelathini ya chaneli za maudhui ya ndani;
(b) kuheshimu haki miliki za ndani na nje ya nchi; na
(c) kuheshimu utamaduni, mila, silka na desturi za kizanzibari.

(2) Mtoa huduma za utangazaji wa kulipia atawapa wateja taarifa zifuatazo kwa maandishi:

(a) aina ya bidhaa, vifurushi na huduma zinazotolewa;
(b) muundo wa gharama wa bidhaa na huduma;
(c) mkataba wa huduma kwa mteja;
(d) bili na ukusanyaji wa ada;
(e) taratibu za kushughulikia malalamiko na utatuzi; na
(f) mbinu za udhibiti wa upatikanaji wa maudhui yasiyofaa kwa watoto.

Wajibu wa mtoa huduma za maudhui ya mtandaoni.

**8.** Mtu anayeishi ndani au nje ya Zanzibar anayeandaa maudhui ya mtandaoni yanayokusudiwa kutumika Zanzibar atakuwa na wajibu wa:

(a) kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria;
(b) kufuata ipasavyo Sheria, Miongozo pamoja na Kanuni zote zilizotolewa na Tume;
(c) kuhakikisha maelezo na taarifa zinazotolewa katika jukwaa la mtandaoni ni sahihi, na ya ukweli;
(d) kuzingatia kikamilifu vigezo vya kitaaluma na maadili ya waandishi wa habari vinavyohitajika katika uwasilishaji wa habari;
(e) kufanya jitihada za kuhariri majadiliano yanayoelekea kuumiza hisia za mtu yeyote kwa kutumia lugha ya kashfa ambayo inaweza kuchochea vurugu, uasi au uvunjifu wa amani;
(f) kuheshimu utamaduni, mila, silka na desturi za kizanzibari;
(g) kuhakikisha kwamba maudhui yaliyotolewa yanakidhi maslahi ya umma, tunu za kitaifa, usalama wa Taifa na umoja wa kitaifa;
(h) kutangaza vipindi ambavyo havichochei masuala ya chuki kwa misingi ya rangi, jinsia, utaifa, dini, ulemavu, umri au ukabila; na
(i) kuepusha kutangaza mambo ya matusi, unajimu, ushirikina kamari, ulevi, vurugu na yatakayosababisha mgawanyiko.

## SEHEMU YA TATU
## MASHARTI YA USAMBAZAJI NA UTENGENEZAJI WA MAUDHUI

Msambazaji wa maudhui.

**9.**-(1) Msambazaji wa maudhui anayekusudia kutoa huduma za maudhui atalazimika kuwa na leseni ya huduma za maudhui.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, msambazaji wa maudhui hatozalisha na kusambaza maudhui yake mwenyewe.

(3) Mwenye leseni ya huduma za maudhui ya utangazaji wa digitali atafanya makubaliano na msambazaji wa maudhui kwa ajili ya urushaji na usambazaji wa maudhui.

(4) Msambazaji wa maudhui hatobadilisha mpangilio wa orodha ya chaneli, kuongeza au kuondosha chaneli bila ya kumuarifu mteja na kutoa taarifa kwa Tume siku saba kabla ya kufanya hivyo.

Masharti ya ujumla.

**10.**-(1) Mtu mwenye leseni atahakikisha kuwa vipindi na uwasilishwaji wake:

(a) vinalinda uhuru wa kitaifa, umoja wa kitaifa, maslahi ya Taifa, usalama wa Taifa na maslahi ya kiuchumi ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla;
(b) vinaakisi utamaduni, mila, silka, maadili na utambulisho wa Mzanzibari;
(c) vinazingatia heshima na adabu na kulinda maadili ya umma;
(d) havitaonesha sura, sauti na kujuulisha mazingira yatakayowezesha kufahamika kwa waathirika wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji;
(e) havitaingilia masuala ya faragha na kushusha hadhi ya mtu binafsi;
(f) vinaepuka matangazo yenye kuhamasisha uchawi, ushindani wa kidini, tiba asilia, unajimu, ushirikina au waganga wa jadi;
(g) vinaepuka kuchochea masuala ya ngono na utupu, matusi, ulevi, kamari, vurugu, ushirikina au unajimu;
(h) vinaepuka kushajihisha ulevi, kamari na matumizi ya dawa za kulevya;
(i) vinaepuka ubaguzi au kudhalilisha watu kulingana na jinsia na havichochei au kuendeleza dharau dhidi ya kundi lolote la watu kwa misingi ya kabila, dini, siasa, asili, ugonjwa au ulemavu;
(j) vinaheshimu hakimiliki za ndani na nje ya nchi;
(k) havina uwezekano wa kuhimiza au kuchochea kutendeka kwa uhalifu au vurugu ikiwemo kuhamasisha mbinu za kujiua, na utengenezaji wa miripuko;
(l) havitaonesha unyanyasaji dhidi ya wanawake na watoto na kuonesha mtazamo kuwa wanawake ni chombo cha starehe;
(m) havitaonesha mbinu au vifaa vya kujeruhi ambavyo vinaweza kuigwa kwa urahisi;

(n) havitaonesha matukio ya picha ya miili au wahanga wa ajali, matukio ya mateso, unyanyasaji wa watu au wanyama, picha za miili ya maiti au maiti zilizochakazwa, watu walio katika maumivu makali au wanaokaribia kukata roho au mapambano ya kikatili bila ya kutoa tahadhari kwa hadhira;
(o) havitajumuisha matumizi ya lugha za kuudhi, ikiwa ni pamoja na matusi, kufuru na hotuba za chuki; na
(p) vitaepuka kutangaza masuala ya kashfa, ubaguzi, uchochezi na lugha zisizo na staha.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) (f) ya kanuni hii, mwenye leseni anayetaka kuwasilisha vipindi au matangazo ya tiba asili na masuala ya dini ataomba kibali kwa mamlaka husika.

Wajibu wa mwenye leseni kulinda mtoto.

**11.**-(1) Mwenye leseni:

(a) atahakikisha kwamba tahadhari inachukuliwa ili kuepuka maudhui ambayo yanaweza kuathiri au kuwa na madhara kwa mtoto;
(b) atazingatia haki za mtoto kwa mujibu wa sheria na mikataba ya kikanda na kimataifa inayohusika;
(c) hatotangaza vipindi vyenye maudhui yasiyofaa kwa mtoto;
(d) ataomba ridhaa kwa maandishi ya kufanya mahojiano na mtoto kwa wazazi au walezi wao; na
(e) atamlinda mtoto dhidi ya vishawishi vibaya vinavyojumuisha matumizi ya madawa ya kulevya, kamari, au masuala ya ngono na utupu.

(2) Kwa mujibu wa kanuni (1) (a) ya kanuni hii, maudhui yenye madhara kwa mtoto ni pamoja na maudhui ya ngono, vurugu, usafirishaji wa mtoto, ajira za mtoto, muziki wenye maneno na vitendo vinavyoashiria ngono, udhalilishaji, ukatili na unyanyasaji kwa mtoto.

Maudhui ya watu wa wazima.

**12.**-(1) Mwenye leseni atahakikisha kuwa maudhui ya watu wazima yanarushwa ndani ya muda wa faragha.

(2) Mwenye leseni, kabla ya kuanza muda wa faragha, atahakikisha kuwa anaitaarifu hadhira.

(3) Mwenye leseni, wakati wa faragha, hatatoa maudhui ya kipindi:
(a) kinachoonyesha matukio ya ngono yaliyowazi;
(b) kinachotoa lugha chafu, matusi na matukio ya vurugu;
(c) kitakachokiuka mila, silka na utamaduni wa Mzanzibari; na
(d) kisichozingatia unyeti wa dini na utamaduni.

Uwasilishaji wa habari.

**13.**-(1) Mwenye leseni ya huduma za maudhui zisizo za kulipia atatenga muda usiopungua saa moja na nusu kwa kila siku kwa ajili ya vipindi vya habari.

(2) Mwenye leseni:

(a) atatoa habari za kitaifa, kikanda na kimataifa;
(b) ataripoti kwa usahihi, umakini, usawa na bila ya upendeleo na ubaguzi wa aina yoyote;
(c) ataripoti habari bila ya kupotosha ukweli uliopo kwa makusudi au kwa uzembe;
(d) hatoruhusu udhamini na matangazo wakati wa taarifa za habari;
(e) atazingatia kikamilifu vigezo vya kitaaluma na maadili ya waandishi wa habari vinavyohitajika katika uwasilishaji wa habari;
(f) atahakikisha mawanda ya habari hayafungamani na msimamo wa kisiasa au kibiashara;
(g) atatoa habari kwa lugha sanifu na sahihi ya Kiswahili au Kiengereza; na
(h) atahakikisha habari anayoiwasilisha inahamasisha mshikamamo, umoja, utaifa na haitumiki katika kudhalilisha, kubagua au kushusha hadhi ya mtu.

Habari za papo kwa papo.

**14.**-(1) Mwenye leseni atahakikisha kwamba, habari za papo kwa papo zinakuwa za kweli na zitatangazwa mara tu zinapotokea.

(2) Bila ya kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, endapo habari za papo kwa papo zinahusisha jambo lenye maslahi ya umma, habari hizo hazitatangazwa mpaka zithibitishwe na mamlaka husika.

Matukio.

**15.** Mwenye leseni atahakikisha kwamba:

(a) anawasilisha kwa kina na kwa uchambuzi wa kitaalamu matukio yakiwemo habari za uchunguzi, makala na mahojiano;
(b) anazingatia kikamilifu vigezo vya kitaaluma na maadili ya uandishi wa habari yanayohitajika katika uwasilishaji wa matukio; na
(c) anazingatia haki na usawa katika uwasilishaji wa vipindi vya matukio.

Utoaji wa maoni binafsi.

**16.**-(1) Endapo mwenye leseni ataruhusu utoaji wa maoni ya mtu binafsi wakati wa kipindi, atawaarifu hadhira mapema juu ya mada itakayojadiliwa na kuwapa fursa ya kushiriki kutoa maoni yao.

(2) Katika utoaji wa maoni binafsi, mwenye leseni ataweka mfumo ambao utawezesha maoni hayo kusubirishwa kwa angalau sekunde kumi na tano kabla ya kurushwa hewani.

Mwenendo wa Baraza la Wawakil ishi na Bunge.

**17.**-(1) Mwenye leseni atahakikisha kwamba:

(a) mwenendo wa Baraza la Wawakilishi na Bunge unaripotiwa kwa usahihi;
(b) hatoi maoni binafsi kuhusu mwenendo wa mashauri ya

vikao vya Baraza la Wawakilishi na Bunge; na

(c) anatangaza vikao vya Baraza la Wawakilishi au Bunge kwa kuzingatia sheria na taratibu za kutangaza vikao hivyo.

(2) Mwenye leseni anayerusha moja kwa moja vikao vya Baraza la Wawakilishi na Bunge hatoruhusiwa kuingiza matangazo wakati wa kipindi hicho au kuonyesha nembo za udhamini.

Mwenendo wa mahakama.

**18.** Mwenye leseni atahakikisha kwamba:

(a) mwenendo wa mahakama unaripotiwa kwa usahihi;
(b) hatoi maoni binafsi kuhusu mwenendo wa mashauri ya mahakama; na
(c) anatangaza mwenendo wa mashauri ya mahakama kwa kuzingatia sheria na taratibu za mahakama.

Matangazo ya biashara.

**19.-**(1) Mwenye leseni atatangaza matangazo ya biashara ambayo:

(a) yameruhusiwa, yenye kuaminika na ya kweli;
(b) yanaendana na kanuni za ushindani wa haki;
(c) hayana maudhui yoyote ambayo yanaweza kupotosha umma, moja kwa moja au kwa taswira yake;
(d) hayashushi hadhi, moja kwa moja au kwa taswira yake, tangazo jengine lolote la bidhaa au biashara;
(e) hayahusiani na pombe, kamari, utupu au masuala ya ngono;
(f) hayahusishi masuala ya ushirikina na unajimu; na
(g) yanafuata mila, silka na utamaduni wa Mzanzibari.

(2) Mwenye leseni hatotangaza tangazo la biashara linalohusiana na tiba mbadala na imani za dini bila ya kupata kibali kutoka kwa mamlaka husika.

(3) Mwenye leseni atahakikisha kwamba:

(a) kabla ya kutangaza tangazo, picha au maelezo yoyote yaliyomo katika tangazo hilo yawe yamethibitishwa na kuidhinishwa na muhusika;
(b) wakati wa kupanga matangazo, anafanya uamuzi yakinifu ili kulinda haki na maslahi ya mtoto;
(c) mtoto hatumiki kwenye matangazo ya biashara yanayoathiri utu wao;

(d) mfanyakazi wa kituo cha utangazaji hatakuwa sehemu ya tangazo la biashara;
(e) sehemu yoyote ya tangazo la biashara inatofautishwa na kipindi kinachotangazwa kwa wakati huo;
(f) kuna tofauti ya wazi ya maudhui ya matangazo ya biashara na vipindi, na atalazimika:
(i) kutenga muda usiozidi dakika tano wa matangazo ya biashara katika kipindi chochote cha dakika thelathini; na
(ii) kuhakikisha kuwa kila tangazo la biashara ndani ya muda

ulioelezwa chini ya aya ndogo ya (i) halizidi sekunde sitini;

(g) tangazo lolote la biashara halihusiani na masuala ya pombe na kamari; na

(h) anazingatia masharti ya Sheria, kanuni, miongozo na maelekezo yoyote yanayohusiana na utangazaji wa matangazo yanayotolewa na Tume.

Habari za biashara.

**20.-**(1) Habari za biashara hazitatangazwa:

(a) kwa zaidi ya muda wa saa tatu na nusu katika vipindi vya kawaida vya siku husika; na

(b) wakati wote wa vipindi vinavyohusiana na mtoto.

(2) Mwenye leseni atahakikisha kwamba habari za biashara:

(a) zinatofautishwa na vipindi vyengine vyovyote vinavyotangazwa kwa wakati huo;

(b) ni halali, ya kweli, ya uaminifu, yenye heshima na inayoendana na kanuni za ushindani wa haki; na

(c) inafuata mila, silka na utamaduni wa Mzanzibari.

(3) Kanuni ndogo ya (1) na (2) za kanuni hii hazitotumika kwa mtoa huduma za utangazaji ambaye hutoa matangazo ya biashara pekee.

Maudhui kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

**21.-**(1) Mwenye leseni atachukua hatua stahiki kuhakikisha watu wenye ulemvu wananufaika na habari pamoja na vipindi vyengine.

(2) Mwenye leseni:

(a) atakuwa mwangalifu wakati wa utoaji wa taarifa au ripoti kuhusu watu wenye ulemavu ili kuhakikisha analinda haki na kuheshimu utu wao;

(b) hatotangaza vipindi vinavyounga mkono na kukuza dhana potofu kuhusu watu wenye ulemavu;

(c) hatorusha vipindi vinavyoonesha unyanyasaji dhidi ya watu wenye ulemavu  na kuonyesha mtazamo kuwa wao ni watu dhaifu na wana haki ya kufanyiwa vitendo vya ukatili; na

(d) atahakisha kwamba watu wenye ulemavu wakiwemo viziwi na wenye usikivu hafifu wanapata ufahamu wa matangazo kupitia lugha za alama.

(3) Mwenye leseni, wakati wa kutangaza taarifa ya habari na matukio, atahakikisha kwamba maudhui yanatoa:

(a) ufafanuzi wa maandishi kwa ajili ya viziwi na wenye usikivu hafifu;

(b) maelezo ya sauti kwa watu wasioona ; na

(c) tafsiri kwa lugha ya ishara.

Maudhui ya elimu.

**22.** Mwenye leseni anayetoa huduma bila ya malipo atahakikisha kuwa kiwango kisichopungua asilimia ishirini ya maudhui yake ya kila siku yawe ni ya elimu.

Kuripoti masuala yenye migogoro.

**23.** Mwenye leseni ya huduma ya maudhui anapokuwa anatangaza masuala yenye migogoro kwa umma, atahakikisha kwamba:

(a) anawasilisha maoni na mitazamo mbalimbali; na
(b) anatoa muda sawa kwa mtu ambaye ameathiriwa na taarifa iliyotolewa kujibu au kukosoa taarifa hiyo ndani ya muda unaofaa.

Mahojiano.

**24.-**(1) Mwenye leseni atahakikisha kwamba mtu yeyote anayehojiwa:

(a) anaarifiwa juu ya mada inayotarajiwa kutolewa katika mahojiano; na
(b) anafahamishwa mapema kuwa mahojiano hayo yanarikodiwa au yanarushwa hewani moja kwa moja.

(2) Mwenye leseni, katika kufanya mahojiano, atazingatia maadili ya kitaaluma ya uandishi wa habari na utangazaji na uzito wa jambo husika.

Katazo kwa mwenye leseni.

**25.** Mwenye leseni:

(a) hatotaja au kuonyesha utambulisho wa muathirika wa udhalilishaji isipokuwa muathirika huyo akikubali kwa maandishi kutajwa utambulisho wake;
(b) hatotaja au kuonyesha utambulisho wa mtoto ambaye ni muathirika wa ubakaji, ukatili, udhalilishaji au uhalifu mwengine wowote; na
(c) ataepuka maelezo ambayo sio ya lazima au yanayojirudia wakati wa kutangaza mazingira ya kosa la ngono.
(d) ataepuka kutumia lugha inayokusudia kupotosha au kusababisha taharuki na mtafaruku;
(e) atachukua tahadhari mahususi ili kuepuka lugha ya kufuru na isiyozingatia maadili, utamaduni na madhehebu ya dini mbalimbali;
(f) ataepuka matumizi ya lugha zisizo na staha na matusi katika uwasilishaji wa vipindi;
(g) ataepuka kutumia lugha isiyofaa, au kuchanganya lugha;
(h) ataepuka kutumia lugha za ishara ambazo zinaweza kuvunja hadhi, haiba na heshima ya mtu; na
(i) atalazimika kutumia lugha sanifu katika uwasilishaji wa vipindi.

Maudhui ya ndani.

**26.-**(1) Mwenye leseni atahakikisha kwamba asilimia sitini ya maudhui yanayosambazwa ni maudhui ya ndani.

(2) Asilimia ya maudhui iliyoainishwa katika kanuni ndogo (1) ya kanuni hii itapimwa kwa kuzingatia wastani wa muda wa vipindi kwa siku

(3) maudhui chini ya kanuni hii yatatayarishwa na:

(a) Mzanzibari au Mtanzania;
(b) mwenye taaluma ya utayarishaji wa filamu na vipindi; na

(c) mwenye leseni iliyoidhinishwa na mamlaka husika kufanya utayarishaji wa maudhui ya ndani.

(4) Kwa madhumuni ya kanuni hii, "maudhui ya ndani" maana yake ni jumla ya vipindi vyote vya televisheni, redio au mitandao ya kijamii ambavyo vitatimiza masharti yafuatayo:

(a) utayarishaji wake uwe kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza;
(b) maudhui yahusu masuala ya kipekee kwa hadhira ya Zanzibar;
(c) angalau asilimia hamsini na moja ya hisa za kampuni ya utayarishaji zinamilikiwa na Mzanzibari;
(d) angalau asilimia sitini ya Wahusika wawe ni Wazanzibari;
(e) sehemu kubwa ya eneo la utayarishaji wa vipindi au filamu iwe Zanzibar au Tanzania; na
(f) mtayarishaji wa vipindi au filamu awe ni Mzanzibari na iwapo watayarishaji ni wengi, asilimia hamsini na moja au zaidi ya watayarishaji hao wawe ni Wazanzibari.

(5) Kwa madhumuni ya kanuni hii, maudhui ya ndani hayahusishi habari na matukio.

(6) Mwenye leseni ya huduma za maudhui ya umma na ya biashara watahakikisha kwamba zaidi ya asilimia themanini ya muziki wao ni muziki wa Zanzibar au Tanzania.

Wajibu wa mtengenezaji maudhui.

**27.-**(1) Mtu yeyote anayeishi ndani au nje ya Zanzibar anayetengeneza maudhui yanayokusudiwa kutumika Zanzibar anapaswa:

(a) kulinda mila, silka na utamaduni wa Kizanzibari;
(b) kuhakikisha maudhui anayorusha hayaleti taharuki wala kuharibu amani, utulivu na usalama wa nchi;
(c) kuhakikisha maudhui anayorusha hayambagui mtu kwa misingi ya rangi, dini au kabila;
(d) atachukua tahadhari mahususi ili kuepuka lugha ya kufuru na isiyozingatia maadili, utamaduni na madhehebu ya dini mbalimbali;
(e) atahakikisha maudhui anayorusha ni ya ukweli; na
(f) ataheshimu haki za watoto, wanawake na watu wenye mahitaji maalum.

(2) Mtengenezaji wa maudhui atakayekiuka Sheria na Kanuni hizi atawajibishwa kwa mujibu wa Sheria na sheria nyengine zinazohusiana na uhalifu wa mitandaoni.

**SEHEMU YA NNE**
**MAADILI YA VIPINDI**

Maadili ya vipindi.

**28.** Maadili ya vipindi iliyoelezewa katika sehemu hii italazimika:

(a) kufuatwa na mwenye leseni yeyote; na

(b) kuzuia utoaji wa maudhui yasiyo ya heshima, uongo, yenye kuonesha ngono utupu na kukiuka mila silka na utamaduni wa mzanzibari.

Matukio yenye maslahi ya Taifa.

**29.**-(1) Utangazaji wa maudhui yanayohusiana na matukio yenye maslahi ya Taifa:

(a) utahakikisha kuwa maudhui kuhusu matukio ya maslahi ya Taifa yanatangazwa mara tu yanapotokea baada ya kuthibitishwa na mamlaka husika; na
(b) utafanywa bila ya malipo pale itakapohitajika kufanya hivyo.

(2) Matukio yenye maslahi ya Taifa yatajumuisha matukio muhimu ya kijamii, kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni au Serikali kwa ujumla yenye maslahi kwa umma.

(3) Hakuna mwenye leseni atakayepata haki ya kipekee ya kutangaza matukio ambayo yana maslahi ya Taifa.

Kutaja jina la kituo na mtayarishaji wa kipindi.

**30.**-(1) Mwenye leseni ya maudhui ya redio atakitambulisha kituo chake na jina la kipindi angalau kila baada ya dakika kumi na tano katika vipindi vyake vya kila siku.

(2) Mwenye leseni ya maudhui ya televisheni atalazimika kuonyesha nembo ya kituo chake muda wote wa matangazo na kutambulisha jina la kipindi.

(3) Mwenye leseni atataja au ataorodhesha majina ya watayarishaji na waongozaji wa kipindi mwanzoni na mwishoni mwa kila kipindi.

Taarifa za uchunguzi.

**31.**Mwenye leseni atahakikisha ripoti za uchunguzi:

(a) zinakuwa na uwiano, sahihi, za haki na kamili na zinashirikisha pande zote zinazohusika;
(b) zinalenga kutoa habari na kuelimisha jamii;
(c) zinahamasisha uwazi, uwajibikaji na utawala bora; na
(d) zinahimiza demokrasia na kupaza sauti za wasio na sauti.

Faragha.

**32.**-(1) Mwenye leseni ya huduma za maudhui hatotangaza mambo yanayohusu maisha ya mtu binafsi ili kulinda haki ya faragha isipokuwa jambo hilo litakapokuwa na maslahi ya kitaifa na limefanyiwa uchunguzi yakinifu.

(2) Mwenye leseni hatotangaza taarifa za kumuudhi au kumkera mtu binafsi isipokuwa kwa jambo ambalo lenye maslahi ya umma.

Vipindi vinavyorushwa hewani moja kwa moja.

**33.**-(1) Mwenye leseni anapotoa maudhui yanayorushwa hewani moja kwa moja:

(a) atakuwa na teknolojia au vifaa vya kiufundi vitakavyomuwezesha kudhibiti maoni yanayotolewa na wasikilizaji na watazamaji kwa njia ya simu au ujumbe mfupi;
(b) atahakikisha kwamba wachangiaji na washiriki wa vipindi wanatendewa haki na hawabaguliwi au kudharauliwa;

(c) atahakikisha kwamba anatii masharti ya sheria za hakimiliki za ndani na nje ya nchi; na
(d) atakuwa huru kuingia makubaliano ya kibiashara ya kuunganisha kipindi na mtoa huduma mwengine.

(2) Mtoa huduma za maudhui anayeunganisha kipindi na kituo chochote cha ndani au nje ya nchi atawajibika kwa maudhui yoyote ambayo hayazingatii matakwa ya Sheria au Kanuni hizi.

Matumizi ya akiliunde.

**34.**-(1) Mwenye leseni anaweza kutumia teknolojia ya akiliunde kama nyenzo ya kumsaidia kutekeleza majukumu yake ikiwemo:

(a) kutafuta mawazo ya habari na kuchakata taarifa;
(b) kutengeneza sauti na picha zinazoendana na maudhui bila ya kuwa na picha halisi za tukio zisizoathiri au kwenda kinyume na maadili;
(c) kufanya utafiti na uchambuzi wa data mbali mbali; na
(d) kufanya uhariri wa vipindi na habari.

(2) Mwenye leseni, ili kuhakikisha matumizi mazuri ta teknolojia ya akiliunde, atapaswa:

(a) kuhakikisha kuwa teknolojia ya akiliunde inatumika kwa uangalifu na kwa kuzingatia maadili ya taaluma ya uandishi wa habari;
(b) kulinda haki ya faragha kwa kufanya utafiti wa kina kabla ya kutoa maudhui yaliyopatikana kwa kutumia kifaa au teknolojia inayoweza kumpatia taarifa za siri au za faragha kuhusiana na taasisi au mtu binafsi;
(c) kuhakikisha kuwa maudhui yaliyopatikana kwa kutumia akiliunde yanazingatia mila, silka na utamaduni wa Kizanzibari;
(d) kuwa na programu maalum za kufundisha watendaji wote wa vituo vya utangazaji namna bora ya kutumia akiliunde katika utekelezaji wa majukumu yao;
(e) kuwa na sera ambayo inatoa miongozo ya matumizi ya akiliunde katika kituo chake;
(f) kutumia akiliunde kama msaidizi na siyo nyenzo pekee ya kufanya kila kitu; na
(g) kuhakikisha hakuna maudhui yanayotangazwa au kurushwa hewani bila ya usimamizi wa awali wa binadamu.

Utazamaji vipindi na familia

**35.**-(1) Mwenye leseni atatoa tahadhahari kwa hadhira kabla ya kuanza kwa kipindi vya watu wazima katika wakati wa kuangalia na kusikiliza vipindi na familia.

(2) Pamoja na tahadhari iliyoainishwa chini ya kanuni ndogo (1) ya kanuni hii, kutakuwa na alama za angalizo zitakazooneshwa kwenye televisheni pamoja na alama za ukomo wa umri, kama ilivyoainishwa chini ya Jadweli la Kwanza la Kanuni hizi.

(3) Tume itatoa muongozo wa muda na matumizi ya alama zilizoainishwa kwenye jedweli la kwanza la kanuni hii.

Ratiba ya vipindi.

**36.**-(1) Mwenye leseni ya huduma za maudhui ataonyesha ratiba ya vipindi vya wiki nzima katika chombo chake cha utangazaji kila siku.

(2) Ratiba ya vipindi iliyoelezwa katika kanuni ndogo (1) ya kanuni hii, itaoneshwa kwa njia ya kielektroniki.

(3) Mwenye leseni atafuata ratiba ya vipindi ambayo ameitowa mapema kwa hadhira aliyoikusudia au watumiaji isipokuwa kama atalazimika kutangaza matukio ya papo kwa papo yenye umuhimu wa kitaifa au kimataifa au kupitia vipindi maalumu vya habari na matukio.

(4) Mwenye leseni atawasilisha Tume:

(a) ratiba ya vipindi vya robo mwaka siku kumi na nne kabla ya kila robo; na

(b) ndani ya siku saba baada ya mwisho wa kila robo, ripoti za utaratibu wa vipindi zinazoeleza idadi ya vipindi vya elimu, watoto na orodha ya kucheza muziki wa ndani iliyotangazwa au kuoneshwa katika robo hiyo.

(5)Mwenye leseni hatobadilisha ratiba ya vipindi bila ya kuiarifu Tume kwa maandishi isipokuwa kwa dharura za umma.

Ubaguzi.

**37.** Mwenye leseni ataepuka:

(a) kutangaza mambo yanayohamasisha ubaguzi na kupandikiza chuki zinazotokana na ukabila, utaifa, asili ya mtu, rangi, dini, jinsia, umri, au ulemavu;

(b) kutumia maneno ya dhihaka, kejeli au mzaha katika kuzungumzia jinsia au kikundi cha kikabila, dini au rangi;

(c) kutumia maneno au ishara za udhalilishaji au kashfa dhidi ya mtu yeyote kwa misingi ya dini, jinsia au ukabila.

(d) kutambulisha kundi la watu kwa utofauti wao wakiwa katika mkusanyiko mmoja; na

(e) kuwaonyesha wanawake kama chombo cha starehe.

Sera ya Uhariri.

**38**.-(1) Kila mwenye leseni za huduma za Maudhui atalazimika kuandaa sera ya uhariri itakayoelezea utaratibu mzima wa utoaji wa maudhui pamoja na uhariri wa vipindi.

(2) Tume itatoa muongozo wa utayarishaji wa sera ya uhariri ambao wenye huduma za maudhui watapaswa kuufata katika kutekeleza majukumu yao ya shughuli za utangazaji.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI MENGINEYO

Dharura za umma.

**39.**-(1) Mwenye leseni atatangaza taarifa ya dharura ya umma na janga la Taifa iliyotolewa na mamlaka husika.

(2) Tume, kwa notisi iliyotolewa kupitia tangazo maalumu la umma, itaelezea utaratibu utakaopaswa kutumika na mwenye leseni katika kutangaza dharura za umma na majanga ya Kitaifa.

**40.** Mwenye leseni anayekiuka masharti yoyote ya Kanuni hizi, ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano za Kitanzania au kifungo cha muda usiozidi miaka miwili au adhabu zote mbili. Uvunjifu wa kanuni.

**41.** Msambazaji maudhui atabeba huduma za utangazaji wa umma, bila ya kutoza ada za urushaji matangazo kwa ajili ya maslahi ya umma. Ubebaji wa huduma za utangazaji wa umma.

**42.** Mwenye leseni ya huduma ya maudhui ya kulipia, atawasilisha Tume uthibitisho wa hakimiliki kwamba anazo haki ya chaneli anazozipitisha katika satalaiti, kebo, au teknolojia mpya zitakazojitokeza. Uthibitisho wa haki.

**43.**-(1) Mwenye leseni aliyepata haki ya kipekee ya kutangaza mubashara matukio ya michezo na mengineyo atazingatia masharti yafuatayo: Masharti kwa ajili ya haki za kipekee.

(a) kwa kuzingatia makubaliano ya hakimiliki kutoka taasisi husika, kuwasilisha Tume nakala ya makubaliano ya kurusha hewani matukio ya mubashara ya michezo wiki tatu kabla ya kuanza kwa kipindi;
(b) endapo mwenye leseni amepata haki ya kutangaza mubashara matukio ya michezo ya nje ya nchi, kuwasilisha makubaliano Tume angalau mwezi mmoja kabla ya kuanza kwa tukio; na
(c) endapo mwenye leseni amepata haki ya kipekee ya kutangaza tukio lolote la michezo mubashara, kuuarifu umma kuhusu haki hiyo kwa kuchapisha katika magazeti matatu yanayosambazwa kwa wingi angalau wiki tatu kabla ya kuanza kwa kipindi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni hii, mwenye leseni aliyepewa haki ya kipekee ya kutangaza mubashara tukio lolote, atazingatia masharti kama yaliyoelezwa chini ya kanuni ndogo (1) ya kanuni hii.

**44.**-(1) Mlalamikaji atawasilisha malalamiko kwa mwenye leseni ndani ya saa arobaini na nane tokea kutangazwa kwa suala linalolalamikiwa. Malalamiko.

(2) Mwenye leseni atayafanyia kazi na kuyatolea uamuzi malalamiko yatakayowasilishwa kwake ndani ya kipindi cha saa sabini na mbili tokea kupokea malalamiko.

(3) Endapo mlalamikaji hajaridhishwa na uamuzi uliotolewa au hakuna uamuzi uliotolewa na mwenye leseni katika kipindi kilichoainishwa, atawasilisha malalamiko kwa Tume ndani ya saa arobaini na nane baada ya uamuzi kutolewa au kushindwa kutolewa.

**45.** Mtoa huduma za maudhui ambaye: Makosa na Adhabu.

(a) amerusha maudhui ambayo yanaleta taharuki na kuharibu amani, utulivu na usalama wa Nchi;
(b) amerusha maudhui ambayo moja kwa moja au kwa taswira yake yana lengo la kumdhalilisha, kumkashifu au kushusha hadhi na heshima ya mtu yeyote;
(c) amerusha taarifa au data iliyowasilishwa katika picha,

maandiko, alama au aina nyingine yoyote ya mfumo wa matangazo ambayo si ya ukweli, udanganyifu, au yenye kupotosha;

(d) ametangaza au kufichua kwa makusudi maelezo ya uchunguzi wa uhalifu ambao unahitaji usiri;

(e) amekiuka masharti ya haki miliki au kurusha kipindi cha mtoa huduma mwengine kwa lengo la biashara au si kwa biashara bila ya ridhaa au makubaliano ya pande zote mbili;

(f) ametumia maneno, amerusha video au ujumbe wowote kwa kuhariri picha ya mtu kwa lengo la kumzihaki, kumchafua au kumshusha hadhi.

(g) amekiuka maadili ya utangazaji kwa mujibu wa kanuni, miongozo iliyotungwa na Tume;

(h) amekiuka kanuni za maadili ya vipindi kwa mujibu wa Kanuni hizi;

(i) ameshindwa kufuata masharti ya ujumla yaliyoelezwa katika Kanuni hizi;

(j) ameshindwa kutekeleza masharti yaliyoambatanishwa katika leseni yake au yaliyomo kwenye kanuni au muongozo wowote uliotungwa na Tume;

(k) ametangaza au kuonesha vitendo vya ngono vya wazi wazi bila ya kuficha taaswira yake;

(l) ametangaza vipindi vinavyoonesha au kuashiria udhalilishaji dhidi ya watoto, wanawake au watu wenye mahitaji maalum;

(m) ametumia lugha ya matusi, kejeli kukashifu, inayoashiria ubaguzi wa aina yoyote;

(n) ametangaza mambo yanayohamasisha ubaguzi na kupandikiza chuki zinazotokana na ukabila, utaifa, asili ya mtu, rangi, dini, jinsia, umri, au ulemavu;

(o) ametangaza au kusambaza kwa mtu mwengine taarifa binafsi za wachangiaji kupitia simu na mitandao ya kijamii;

(p) ametoa maudhui yaliyopatikanwa kwa kutumia akiliunde bila ya kuzingatia mila, silka na utamaduni wa Kizanzibari;

(q) amekataa kutoa haki ya kujibu kwa mujibu wa Sheria, kanuni na miongozo iliyotolewa na Tume;

(r) ametangaza vipindi bila ya kufuata mpangilio wake wa vipindi ulioindhinishwa na Tume; au

(s) amekiuka Sheria, kanuni, miongozo na maelekezo yaliyotolewa na Tume,

ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Uwezo wa kumaliza kosa.

**46.** Endapo mtoa huduma wa maudhui amekiuka masharti ya Kanuni hizi, Katibu mtendaji anaweza, kwa mujibu wa taratibu zilizoelezwa chini ya Kanuni hizi, kumaliza kosa lililotendwa.

Utaratibu wa kumaliza kosa.

**47.**-(1) Kwa kuzingatia uwezo chini ya kanuni ya 47, Katibu Mtendaji atampa mtu huyo, notisi iliyoainishwa chini ya Jadweli la Pili la Kanuni hizi, itakayomtaka mtu huyo kulipa faini kulingana na kosa alilotenda.

(2) Notisi chini ya kanuni ndogo (1) ya kanuni hii, itaanisha:

(a) jina na anwani ya mtu;
(b) tarehe na eneo la kosa lilipotokea;
(c) kosa lililoshutumiwa kutendwa;
(d) eneo na muda ambao kosa limetendwa;
(e) kiwango cha faini kitakachotakiwa kulipwa kwa kosa hilo;
(f) muda na namna ambayo faini italipwa; na
(g) taarifa au maelezo mengine yoyote yanayohusiana na kosa hilo kama Katibu Mtendaji atakavyoona muhimu.

(3) Mtu aliyepewa notisi chini ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, ndani ya siku saba kutoka siku ambayo notisi imepokelewa, atalipa kiwango cha faini kwa Tume.

(4) Endapo mtu ambaye amepewa notisi chini ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, atashindwa kulipa kiwango cha faini kilichoainishwa ndani ya muda wa notisi, Katibu Mtendaji ataendelea kuchukua hatua za kisheria dhidi ya mtu huyo.

(5) Endapo mtu atalipa kiwango cha faini kilichoainishwa ndani ya notisi, hakuna hatua za kisheria zitakazochukuliwa kuhusiana na kosa hilo kwa mtu huyo.

**48.** Endapo mlalamikaji au Mwenye leseni hajaridhishwa na uamuzi wa Tume anaweza kukata Rufaa kwa Baraza la Ushindani halali wa Biashara la Zanzibar. Rufaa.

**JADWELI LA KWANZA**

**UTIZAMAJI WA VIPINDI NA FAMILIA**

**[Chini ya kanuni ya 35(2)]**

---

| **ALAMA ZA ANGALIZO ZITAONESHWA KWENYE TELEVISHENI** | | |
|---|---|---|
| **Na.** | **Alama za angalizo** | **Maana ya alama** |
| **1.** | “L” | Kwa maudhui ambayo yatakuwa na lugha ya kukera japo kwa kiwango kidogo. |
| **2.** | “C” | Kwa maudhui ambayo yatakuwa na picha za kukirihisha. |
| **3.** | “V” | Kwa maudhui yanayoonesha ukatili. |

| **ALAMA ZA ANGALIZO KWA UKOMO WA UMRI** | | |
|---|---|---|
| **Na.** | **Alama za angalizo** | **Maana ya alama** |
| **1.** | “18+” | Kwa maudhui ambayo yanaruhusiwa kuangaliwa kwa mtu mwenye umri wa miaka kumi na nane au zaidi. |
| **2.** | “16+” | Kwa maudhui ambayo yanaruhusiwa kuangaliwa kwa mtu wenye umri wa zaidi ya miaka kumi na sita. |
| **3.** | “13+” | Kwa maudhui ambayoyanaruhusiwa kuangaliwa kwa mtu mwenye umri wa zaidi ya miaka kumi na tatu. |
| **4.** | “FAM” | Kwa maudhui ambayo yanafaa kuangaliwa kwa familia. |
| **5.** | “PGA” | Kwa maudhui ambayo yanafaa kuangaliwa kwa usimamizi wa wazazi au walezi. |

**JADWELI LA PILI**

**NOTISI YA KUMALIZA KOSA**

**[Chini ya kanuni ya 47(1)]**

---

**A: TAARIFA ZA ALIYEFANYA KOSA**

Jinakamili…………………………………………………………………………

Tarehe……………………………………………………………………………..

Aina ya kosa lililofanywa ……………………………………………………….

Mahali na wakati wa
kosalililotendwa………………………………………………..

**B: AINA YA FAINI**

Idadi ya makosa yaliyotendwa
………………………………………………………

Faini ya Shilingi za
Kitanzania……………………………………………………..

Taarifa zingine (kama zipo)
…………………………………………………………

**C: TAMKO**

Mimi ………………………. kutangaza kwamba, taarifa zote zilizomo humu ni za kweli kwa kadri nijuavyo. Kwa hiyo, ninajitolea kutii notisi hii na niko tayari kulipa Tsh………………………….. kama faini kwa kosa lililoainishwa katika notisi hii.

Jina ……………………………………….….…………

Sahihi……………………………………………………

Tarehe……………………………………………………

**D: KWA MATUMIZI YA OFISI PEKEE**

Jina la Keshia/wakala anayetoa

notisi……………………………………………………………..……………

Tarehe………………………………………………………………………

Sahihi………………………………………………………………………

Jina la Afisa Msimamizi /wakala anayetoa faini ………………………..……

Tarehe………………………………………………………………………

Saini…………………………………………………………………..….…

Muhuri……………………………………………………………………...…

Katibu Mtendaji Tume ya Utangazaji

**ZIMETIWA** saini tarehe 31 Julai, 2026.

**DKT. RIZIKI PEMBE JUMA**
**WAZIRI WA HABARI, SANAA, UTAMADUNI**
**NA MICHEZO**
**ZANZIBAR.**

*LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR 2026*